Jina: . …….. **Shule……**

Nambari . ……..……

Karatasi hii ina kurasa nne zilizopigwa chapa. Mtahiniwa ahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo , Tanbihi: Mwanafunzi afuate masharti. Akijibu zaidi ya maswali manne swali la mwisho halitasahihishwa

1. (Lazima)

Soma shairi hili kasha ujibu maswali yanayofuata

1.	Mkono inuka	inuka hima	twaa kalamu
	Upate ya'ndika	kwa khati njema	hino nudhumu
	Ipate someka	wenye kusoma	waifahamu
	Wapate yashika	na kuyapima	yaliyo humu
2.	Kuandika anza	anza 'sikawe	mkono wangu
	Na mimi naanza	kisa chenyewe	cha mlimwengu
	Alivyonifanza	nao wajuwe	waja wenzangu
	Wapate jitunza	Salama wawe	hawa ndu zangu
3.	Mja sikudhani	Sikudhaniya	'tanizunguka
	Nikamuamini	nafikiriya	hatageuka
	Kumbe mwafulani	hakuzoweya	kuaminika
	N'shambaini	ingawa baya	lishanifika
4.	Menitenda kisa	Kisa adhimu	mja mcheni
	'mezinduka sasa	n'shafahamu	najuwa kwani
	Ni yangu makosa	najilaumu	kumuamini
	Sikuwa napasa	hata sehemu	kumthamini
5.	'meniuwa mja	mja ni nduli	tahadharini
	Mjaye daraja	nda kikatiki	hana imani
	Muonapo mja	kaani mbali	mujitengeni
	Asiye akaja	kwani habali	kuhasirini
6.	Mja hana haya	haya hazimo	mwake usoni

Mja ni mbaya	hutimba shimo	ungiye ndani!
Na ukishangiya	azome zomo	furaha gani!
Mmoja kwa miya	ndiye hayumo	baya kundini

Maswali

(a) Eleza bahari mbili zinazoafiki mtungo huu. (alama 2)

(b) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari (alama 4)

(c) Fafanua uhuru wa kishairi uliotumiwa na mshairi. (alama 2)

(d) Chambua umbo la shairi hili. (alama 4)

(e) Eleza maudhui ya shairi hili. (alama 4)

(f) Ni nini maana ya maneno haya. (alama 4)

(i) waja

(ii) nduli

(iii) twaa

(iv) hutimba

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA: Kifo Kisimani

Jibu swali la 4 au la 5

4. a) Eleza chanzo cha kufarakana kwa wahusika mbalimbali katika tamthilia ya Kifo Kisimani. (alama 10)

b) Mwandishi wa Kifo Kisimani ameendeleza uhalisia wa mambo katika jamii. Kwa kutoa mifano unga mkono kauli hii. (alama 10)

5. “Usiendelee kunikasirikia mama! Msimamo wangu kumhusu ……. umebadilika. Nimegundua…..”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Eleza sifa na umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)

c) Fafanua jinsi maudhui ya usaliti yalivyoendelezwa katika tamthilia hii. (alama 10)

HADITHI FUPI

K.W. WAMITILA: Mayai Waziri wa Maradhi

6. a) Hadithi ya Msamaria Mwema imejaa kinaya. Eleza. (alama 10)

b) Taja na ufafanue namna sanaa imetumiwa katika kisa hiki. (alama 5)

c) Eleza mambo muhimu yanayojadiliwa kwenye kisa hiki. (alama 5)

FASIHI SIMULIZI

7. a) Maigizo ni nini? (alama 2)

b) Eleza aina na sifa za maigizo unazojua. (alama 6)

c) Fafanua dhima ya maigizo katika jamii. (Alama 12)

Mwisho